*Mulika, Na. 44 (1), 60-73*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*

# Mdhihiriko wa Kani ya Ardhi katika Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla: Uchanganuzi wa Kiontolojia

*Tatu Y. Khamis*[1] *na Aginiwe N. Sanga*[2]

DOI: https://doi.org/10.56279/mulika.na44t1.4

**Ikisiri**

Makala haya yanahusu mdhihiriko wa kani ya ardhi katika riwaya teule za Muhammed Said Abdulla kwa kuzingatia uchanganuzi wa kiontolojia. Ardhi ni kipengele cha kiontolojia chenye kani kubwa katika jamii za Kiafrika (Khamis, 2022). Inaaminika kuwa ardhi ina uhusiano wa moja kwa moja na maisha ya mwanadamu; yaani ina uwezo wa kuzalisha, kuendeleza na kumaliza uhai wa watu katika jamii husika (Hassan, 2018). Makala yametumia riwaya teule za Muhammed Said Abdulla kudhihirisha kuwapo kwa fikra kuhusu kani ya ardhi katika jamii za Kiafrika. Hivyo, hoja kuu ya makala haya ni kwamba katika riwaya teule za Muhammed Said Abdulla (kuanzia sasa MSA) kunadhihirika kani ya ardhi kiontolojia. Kani hizo zinapatikana katika maeneo, mapambo na matumizi yake. Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika. Data za makala haya zimepatikana maktabani. Mbinu iliyotumika kukusanyia data ni uchambuzi wa matini. Mjadala ulifanyika kwa kuegemea katika riwaya tatu za MSA ambazo ni *Kisima cha Giningi* (1958), *Duniani Kuna Watu* (1973) na *Kosa la Bwana Msa* (1984). Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa ardhi ina kani kiontolojia kupitia vipengele vya maeneo na sifa zake, mapambo ya ardhi na matumizi ya ardhi.

## 1.0 Utangulizi

Makala haya yanajadili kani ya ardhi katika riwaya teule za MSA kiontolojia. Kani ni nguvu inayotokana na msukumo wa kitu fulani (BAKIZA, 2010:144; BAKITA, 2017:389). Hii ina maana kwamba kitu huwa na nguvu itokanayo na hali ya utendaji wa jambo husika. Aghalabu, kani huwa kitu kisichoonekana (Kamage, 2023). Hudhihirika kupitia kuwapo kwa utendaji wa mfumo fulani katika maisha ya jamii husika (Ngangah, 2019). Pia, kani hudhihirika kupitia vipengele mbalimbali ikiwamo ardhi. TUKI (2019:202) inafafanua ardhi katika namna mbili: mosi, ardhi ni nchi kavu; na pili ni dunia. Hapa ndio kusema kuwa ardhi ni sehemu ya dunia ambayo inahusisha nchi kavu. Hivyo, katika makala haya unapojadiliwa mdhihiriko wa kani ya ardhi, inakusudiwa nguvu iliyomo katika ardhi inayodhihirisha kuwapo kwa maisha ya mwanadamu na mazingira yanayomzunguka.

[1] Mhadhiri, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania. Baruapepe: khamist910@gmail.com
[2] Mhadhiri Mwandamizi, Chuo Kikuu cha Dodoma, Tanzania. Baruapepe: Aginiwe.sanga@udom.ac.tz

Kimsingi, ardhi ni rasilimali muhimu katika maisha ya mwanadamu, ambayo hujumuisha sehemu inayoonekana na isiyoonekana (Hassan, 2018). Kwa mwanadamu, ardhi ni miongoni mwa vipengele vinavyotambulisha kuwapo kwake. Hii ni kwa sababu ardhi ina nguvu kubwa katika kuwapo kwa uhai wa maisha ya mtu (Ponera, 2023). Hivyo, ardhi ni kitu chenye thamani inayobainika kupitia matembezi kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Kwa mujibu wa Ponera (2023), ardhi ni zawadi kutoka kwa Mungu ambayo mwanadamu huitumia kuendesha maisha yake ya kila siku. Hivyo, huthaminiwa na mwanadamu kama chanzo cha utajiri, nyenzo ya kuendeleza maisha yake baada ya kifo, kurahisisha mawasiliano baina ya waliokufa na walio hai, na kudumisha mtiririko wa kani-uhai kupitia matambiko. Kwa mantiki hiyo, thamani ya ardhi, huonekana kupitia kani inayodhihirika kiontolojia (Mulokozi, 2017).

Ontolojia ni dhana inayorejelea kuwapo kwa mtu, jamii na ulimwengu kwa jumla, sababu na hatima yake (Temples, 1959; Mbiti, 1969; Chuachua, 2016; Mulokozi, 2017). Akizungumzia kuhusu ontolojia ya mtu, Ponera (2023) anasema kuwa mtu hupambanuliwa na moyo, jina na ardhi. Hivyo, ontolojia hushughulikia kuwapo kwa viumbe vinavyoonekana na visivyoonekana, pamoja na maumbile ya ulimwengu (Khamis, 2021). Kiasili, ontolojia inahusishwa na utashi wa mwanadamu pale alipoanza kuathiriana na mazingira yake (Carazzon, 2010). Kutokana na hili, mazingira ndio msingi wa kumpambanua mtu ili kukamilika ontolojia yake. Mor (2001) anataja baadhi ya vipengele vya kimazingira vinavyokamilisha ontolojia ya mtu ambavyo ni makazi, tajiriba, mila, desturi na ardhi.

Hata hivyo, tafiti ambazo tayari zimekwishafanyika kuhusu kani ya ardhi hazijakitwa katika misingi ya kinadharia ya Ontolojia ya Kiafrika, hivyo, hufinya kueleweka kwa upana wake kiontolojia. Mpalanzi (2019) anapozungumzia masuala ya nguvu-uhai katika fasihi ya Kiswahili, anaeleza kuwa kunahitajika tafiti za kina kuhusu nguvu uhai ili kuweza kueleweka vyema. Kutokana na hali hii, makala haya, yanadhihirisha kani ya ardhi kiontolojia kupitia vipengele vya maeneo na sifa zake, mapambo na matumizi ya ardhi ili kuweka wazi upana na nguvu-hai kama inavyobainika katika jamii za Kiafrika.

## 2.0 Methodolojia

Utafiti huu ulisanifiwa kiuchunguzi kifani. Usanifu huu huwezesha kutafiti jambo kwa kina kwa kuweka wazi mfumo au mifumo iliyofungwa katika muda maalumu kupitia ukusanyaji wa kina wa data wenye kujumuisha vyanzo vingi vya taarifa ili kupata maana (Creswell, 2002; Mwinyi, 2020). Uchunguzi kifani wa kitaamuli ulitumika kwa sababu ulisaidia kukusanya taarifa za kina katika uhalisi wake (Cohen na wenzake, 2007). Aidha, uliruhusu kupambanua na kufasili maana ya data zilizopatikana kwa kuzingatia amali na thamani za jamii, mielekeo na fikra zao (Guba na Lincon, 1981; Merriam, 1998; Mwinyi, 2020). Kwa ujumla,

uchunguzi kifani wa kitaamuli ulisaidia kupata undani wa mdhihiriko wa kani ya ardhi katika riwaya teule za MSA kiontolojia. Data za makala haya kwa kiwango kikubwa zimetokana na utafiti wa maktabani. Data za msingi zilipatikana kwa kutumia njia za uchambuzi wa matini. Jumla ya riwaya teule tatu (3) za Muhammed Said Abdulla zilisomwa na kuchambuliwa. Riwaya hizo ni *Kosa la Bwana Msa* (1984), *Duniani Kuna Watu* (1973) na *Kisima cha Giningi* (1958). Data zimewasilishwa na kujadiliwa kwa kutumia mbinu ya usimbishaji wa kimaudhui. Matokeo yamejadiliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maelezo kwa kuzingatia misingi ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika.

## 3.0 Nadharia Iliyotumika

Ontolojia ya Kiafrika ni nadharia inayofungamana na kani uhai inayohusishwa na Mungu, miungu, mwanadamu na jamii. Mwasisi wa nadharia hii ni Placide Tempels (1945). Baadaye, wataalamu kama vile Kagame (1956), Mbiti (1969), Kezilahabi (1985), Makumba (2005), Mihanjo (2004), Mulokozi (2017) na Kaponda (2018) waliiendeleza nadharia hii katika namna mbalimbali (Khamis, 2022). Misingi ya nadharia hii ni: mosi, dhana ya familia pana inayojumuisha waishio sasa, waliofariki na ambao hawajazaliwa; pili, suala la imani ya kuwapo kwa ulimwengu wenye matabaka matatu, yaani duniani, kuzimu na mbinguni; tatu suala la kuheshimu wahenga[3]; nne, kuthamini uzazi kwa kuamini kuwa ndiyo njia ya uzima wa milele na ugumba ni laana; msingi wa tano ni imani kuhusu kuwapo kwa kani inayohusishwa na Mungu Mkuu, miungu, mwanadamu na mizimu ambayo huambatana na imani katika sihiri na uganga. Aidha, msingi wa sita ni dhana ya wakati na ujamiishaji kuwa wa mduara. Katika makala haya, msingi wa kuwapo kwa kani inayohusishwa na nguvu ya Mungu Mkuu, miungu, mwanadamu, na mizimu ndio uliotumika, kwa sababu kani ya ardhi kama kipengele cha ontolojia ya Waafrika kinaongoza maisha ya jamii inayoizunguka.

## 4.0 Yaliyomo katika Riwaya Teule za MSA kwa Muhtasari

Sehemu hii inatoa mihtasari ya riwaya teule za MSA ambazo ni *Kosa la Bwana Msa*, *Kisima cha Giningi* na *Duniani Kuna Watu*.

### 4.1 Muhtasari wa Riwaya ya *Kosa la Bwana Msa*

*Kosa la Bwana Msa* ni riwaya iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1984. Toleo lililotumiwa katika makala haya ni la mwaka 2013 ambalo limechapishwa na Vide~Muwa Publishers Ltd. Riwaya hii ni miongoni mwa riwaya pendwa ambazo maudhui yake kwa kiasi kikubwa yanahusu masuala ya dini, mapenzi na ndoa, wivu na upelelezi. Masuala hayo yamejadiliwa kupitia wahusika kama vile Bwana Msa, Jamila, Bwana Seyyid Ahmed (Bwana Ali Soud), Tunu, Bi. Shinuna

[3] Wahenga ni watu waliokufa miaka mingi. Miongoni mwa sifa zao ni kuwa na athari kwa walio hai kutokana na imani kuwa roho zao bado zinaishi. Pia, ni chanzo cha maarifa ya asili ya Wabantu na ndiyo kiungo kati ya Wabantu na Mungu wao (Chuachua, 2016).

na Sheikh Judi. Kwa upande wa mapenzi, tunamwona Seyyid Ahmed alivyokuwa akimpenda Jamila, kiasi ambacho hata kulala alikuwa hawezi kama hajawasiliana naye. Aidha, wivu unajidhihirisha pale ambapo Bi. Shinuna anakwenda kumtusi Jamila baada ya kugundua kuwa ameolewa na mume wake, Seyyid Ahmed, kwa kificho, mume ambaye alitumia jina bandia akijiita Bwana Ali bin Soud. Hapo ndipo suala la upelelezi linapoanza kwa kutaka kugundua ikiwa Seyyid Ahmed ndiye Bwana Ali bin Soud.

### 4.2 Muhtasari wa Riwaya ya *Duniani Kuna Watu*

*Riwaya ya Duniani Kuna Watu* kwa mara ya kwanza ilichapishwa mwaka 1973. Toleo lililotumika katika makala haya limechapishwa mwaka 2017 na East African Educational Publishers Ltd. Riwaya inahusu maisha ya Bw. Hakimu Marjani na familia yake yenye watoto wawili, Kasim na Selume.

Bw. Hakimu Marjani aliweka alama katika aya za msahafu na akaupeleka kwa Bi. Mariamu Mkebe, ambaye alimuoa kwa jina la Abdulla na kuzaa naye mtoto moja, ambaye ndiye Saleh. Ndani ya msahafu huo, Bw. Hakimu aliandika kumbukumbu ya tarehe ya kuzaliwa Selume, tarehe ya kuzaliwa Saleh pamoja na tarehe ya kufunga ndoa yake. Riwaya hii imejikita katika kuzungumzia chimbuko halisi la familia ya Bw. Hakimu, ujio wa Kasim, Saleh na asili ya Bwana Hakimu. Pia, inaelezea sababu ya Bw. Hakimu kutambulika kwa majina mawili tofauti, yaani, Hakimu Marjani (jina lake halisi) na Abdulla (alilojipa wakati wa kumuoa Bi. Mariamu Mkebe).

### 4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Kisima cha Giningi*

Riwaya ya *Kisima cha Giningi* ilichapishwa kwa mara ya kwanza na Evans Brothers Kenya Limited nchini Kenya, mwaka 1968. Toleo lililotumika katika makala haya limechapishwa mwaka 2011. Riwaya inahusu maisha ya watu wa Giningi ambao wanaamini juu ya kuwapo kwa Mwenyezi Mungu. Watu hawa wana tabia ya kupenda mali za kurithi kuliko utafutaji wa mali kibinafsi. Harakati za maisha katika kijiji cha Giningi zinasababisha Mwana wa Giningi kupoteza maisha yake akiwa kwenye kisima cha Giningi. Wapelelezi wanafanya kazi ngumu ya kumbaini mhusika. Hata hivyo, Bwana Msa anafanya kazi ya ziada juu ya suala hili akishirikiana na Spekta Seif na askari wengine. Hatimaye, wanafanikiwa kumpata mhusika wa mauaji ya Mwana wa Giningi. Inabainika kuwa, Ali Makame, baba yake mdogo Mwana wa Giningi, ndiye aliyehusika na mauaji kwa sababu ya tamaa zake za kumiliki mali yote ambayo Mwana wa Giningi aliachiwa na baba yake.

## 5.0 Kani ya Ardhi Kiontolojia

Sehemu hii inabainisha uchimuzi wa kani ya ardhi kama ilivyosawiriwa katika riwaya teule kiontolojia. Utafiti umebaini kuwa kiontolojia, kani ya ardhi inabainika kupitia maeneo na sifa zake, mapambo ya ardhi na matumizi.

## 5.1. Maeneo katika Ardhi na Sifa zake

Fikra za kiontolojia zinatutanabahisha kuwa, kuna kani ya uhai inayohusishwa na Mungu Mkuu, miungu, mwanadamu na mizimu ambayo inadhihirisha kuwapo kwa kani za kiontolojia katika kipengele cha ardhi (Khamis, 2022). Hii ni kusema kuwa fikra hizo zinahusishwa moja kwa moja na kuwapo kwa maisha ya watu katika jamii husika. Hili linathibitishwa na Ponera (2023) anapozungumzia juu ya mtu ni ardhi, anaeleza kuwa suala la ardhi lina nafasi kubwa katika uwazaji wa Wabantu na ulimwengu wao kwa jumla. Kwa kuwa mwandishi MSA, aliifahamu vyema kani ya ardhi ya jamii yake, anaeleza kwa undani maeneo ya miji na sifa za miji hiyo kama ilivyo ili kuthibitisha kuwapo kwake. Hii ni kusema kuwa katika riwaya za MSA, kuna mdhihiriko wa kuwapo kwa kani ya ardhi kutokana na kuwapo kwa maeneo ya ardhi hiyo na sifa zake. Kwa mfano, katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, mwandishi anaelezea maeneo ya Chakechake na Pemba, kwa kusema:

> Bwana Msa alirudi Pemba jana usiku, mwili wake wote umechoka kwa nyendo nyingi alizokuwa nazo huko; kupanda vilima na kushuka mabonde, hasa kule alikofikia yeye, Chakechake, ambako ardhi yake yote ni "pandashuka" – ama ni vilima au ni mabonde (uk. 39).

Dondoo hili linaonesha jinsi ardhi ya Zanzibar ilivyo na vilima na mabonde ya hapa na pale, hasa katika kisiwa cha Pemba. Hivyo, kuwapo kwa maeneo hayo ni uthibitisho wa kuwapo kwa kani ya kiontolojia katika jamii ya Wazanzibari. Uthibitisho huu unadhihirika kupitia maeneo yenye miinuko, ambayo aghalabu hukaliwa na watu kwa ajili ya shughuli zao za kilimo. Hivyo, nguvu ya uzalishaji husababishwa na ardhi yenye hali kama hiyo.

> Kutokana na maelezo ya dondoo lililotolewa, fikra za kiontolojia kuhusu kani ya ardhi zinadhihirishwa na miji na vijiji ambavyo vinasadifiwa kwa majina pamoja na mazingira yake. Halikadhalika, miji hiyo inasadifu watu wake kwa matamshi, hulka, kilimo, historia na maingiliano yao. Suala hili linaashiria kwamba, kani ya ardhi ni sehemu muhimu ya kutambulisha kuwapo kwa Wazanzibari. Hii ni kwa sababu Wazanzibari, kama watu wa maeneo mengine katika Afrika, hutambuliwa kutokana na sifa walizo nazo ambazo zinatofautiana na watu wengine kutokana na namna fikra zao zilivyoathiriwa na epistemolojia yao, ambayo ndiyo iliyozaa kuwapo kwao (Khamis, 2022). Kutokana na fikra za Wazanzibari kuhusu maeneo yenye miinuko ni kwamba, hayo ni maeneo yenye rutuba na

> mvua za kutosha. Hivyo, ni maeneo bora ya kuishi kwa sababu yanasaidia katika uzalishaji na kipato. Kwa ujumla, kani ya ardhi inadhihirika kiontolojia kutokana na fikra kuhusiana na masuala ya kiroho pamoja na uhai wa jamii kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu kama inavyotiliwa nguvu na msingi wa ontolojia ya Kiafrika.

Aidha, mwandishi ametaja maeneo mbalimbali ambayo yanajulikana kwa sifa zake. Kwa mfano, ametaja maeneo ya mjini Unguja kama vile Hurumzi (kur. 3, 41), Mtendeni (uk. 6), Shangani (kur. 18, 95), Mambo Msiige (uk. 18), Mnazi Mmoja (uk. 54), Mkunazini (uk. 54), Malindi (uk. 69) na Vuga (uk. 71). Pia, ametaja maeneo ya shamba kama vile Kazole (uk. 53). Madondoo yote hayo yanaonesha kuwapo kwa kani ya ardhi ambayo kwayo ina maeneo tofautitofauti yenye sifa lukuki na mapambo kadhaa. Akizungumzia kuhusu maeneo ya miji, Ameir (2011) anasema kuwapo kwa Wazanzibari kunaoneshwa na ule uhalisi wa mitaa na matukio ambayo ni maarufu katika mitaa hiyo. Kwa mfano, mtaa wa Kwahani una walevi, wizi, masuala ya ujambazi, kamari na mambo mengine mengi yafananayo na hayo. Majestiki inaonekana ni sehemu za starehe, na sinema ambazo mpaka sasa zipo. Hii inamaanisha kuwa kule kuonesha uhalisi wa mitaa na matukio, kunathibitisha kuwapo kwa ardhi ya Wazanzibari. Kiontolojia kuwapo kwa sifa za miji katika ardhi ya Wazanzibari, kunatokana na fikra za wanajamii kuwa, mitaa hiyo wanaishi watu wasiojiegemeza katika maamrisho ya nguvu za Mwenyezi Mungu. Kwa upande wa matukio na masuala ya starehe na mambo mengine ya anasa ni kutokana na fikra kuwa mwanadamu anatakiwa aishi kama vile atadumu milele. Hivyo, starehe ni sehemu ya maisha ya kila siku. Maelezo haya yanadhihirisha kwamba kama ardhi ya jamii ya Wazanzibari isingekuwa na nguvu kiontolojia, kusingepatikana watu wenye sifa hizo katika maeneo husika. Hili linashadidiwa na Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika ambapo majina ya vitu yana maana katika nguvu asili ya Mungu iliyomo katika vitu hivyo. Akiunga mkono hoja hii, Kamage (2023) anasema jina la kitu chochote kisicho na uhai au kitu cha asili, huweza kutumika kuelezea nguvu zisizoelezeka za Mungu ambazo hupitishwa katika kitu hicho.

### 5.2 Mapambo ya Ardhi

Mapambo ni wingi wa pambo ambalo ni neno linalorejelea kitu au kifaa kinachotumika kupamba au kuongeza urembo au uzuri kwa mtu, nyumba au katika kitu kingine chochote (TUKI, 2017). Kwa maana hiyo, mapambo ya ardhi inayozungumziwa katika makala haya yanarejelea jumla ya vitu vyote vinavyotia uzuri katika ardhi. Hassan (2018) akizungumzia suala la ardhi katika ujaala wa kijadi, anasema ujaala huo unatumia mapambo ya ardhi kama vile makaburi, miti mikubwa, milima, mapango, na mikusanyiko ya maji (bahari na mito). Kwa fikra za kiontolojia, vitu hivi vina nguvu ambazo watu huzitumia katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Katika riwaya teule kunadhihirika mapambo ya ardhi kama vile miti, mito, mapango, mashamba na bahari. Imebainika kuwa wanajamii

wa Zanzibar wanaamini kuwa kila pambo lina umuhimu wake katika ardhi yao. Inaaminika kuwa kila kiumbe kinachoishi, kwao kina makazi na chakula kutokana na mapambo yanayopatikana katika ardhi yao. Umuhimu wa miti ni pamoja na kupata matunda, mbao, vivuli, makazi ya baadhi ya ndege na hata ibada (Khamis, 2022). Mathalani, kuhusu nguvu katika miti, fikra za kiontolojia ni kwamba miti hiyo ina uwezo wa kutatua matatizo mbalimbali. Hii ni kwa sababu miti ina nguvu-uhai inayowezesha kufanikisha haja na masuala mbalimbali ya jamii husika. Hili linathibitishwa na Hassan (2018) kwa kusema kuwa miti hufungamanishwa na uwezo wa kumsaidia mwanadamu katika maisha yake. MSA anasawiri mazingira ya miti ilivyo katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu* kwa kudhihirisha kuwapo kwa pambo hilo katika jamii za Wazanzibari. Anasema:

> ...Kwa mbele kidogo, ulikuwapo mzeituni na baada ya mzeituni waliliona jabali au jiwe kubwa lililojitandaza mbele yao kiasi cha yadi kumi kwa urefu na limekwenda juu kiasi cha yadi tano. Mbavuni kwake na hata kileleni juu, mmeotea miti mwitu yenye matawi membamba, marefu, na majani yake mapana. Miti hiyo ilifunika kabisa hilo pango lililomo katika lile jabali, hata ikawa kama mtu si mwenyeji hawezi kabisa kuliona au kukisia kuwa pana pango au tundu lolote (uk. 63).

Dondoo hili linaifafanua miti ambayo hujitokeza katika ardhi za jamii ya Wazanzibari. Miti hiyo, mara nyingi, hutumika kwa shughuli mbalimbali ambazo hujidhihirisha kama kani ya kiontolojia katika jamii husika. Kufafanuliwa namna miti ilivyo katika sehemu ya pango, kunadhihirisha nguvu iliyopo katika miti hiyo. Hii ni kusema kuwa, kwa jamii ya Wazanzibari, miti huwa na nguvu za kuweza kutatua mambo mbalimbali yanajitokeza miongoni mwa wanajamii. Ndiyo maana Bw. Hakimu alitumia sehemu yenye miti kuficha mali zake kwa imani kuwa nguvu zilizopo katika sehemu hiyo yenye miti zinalinda mali hizo.

Mapambo mengine yanayotumiwa ni mapango. Haya yana umuhimu sana kwa Wazanzibari kwa sababu hutumiwa kwa kujisitiri, kuficha mali, na makazi ya baadhi ya jamii (Khamis, 2022). Pango ni uwazi mkubwa ulioko katika ardhi au miti mikubwa (Hassan, 2018). Fikra za kiontolojia kuhusu imani ya kani ya mapango ipo katika imani kuwa katika mapango kuna nguvu inayolinda, kuhifadhi na kuhuisha uhai kwa watu katika jamii husika. Mathalani, katika mapango ya Amboni yanayopatika katika mkoa wa Tanga, nayo yanahusishwa na imani hii kwa baadhi ya watu kwa sababu huyatembelea kwa lengo la kufanya ibada zao (Hassan, 2018). Katika riwaya ya *Duniani Kuna Watu*, MSA amelionesha hili pale Bw. Marjani alipokwenda kuficha mali zake katika pango la Kazole ili zisije zikaibiwa, mpaka pale watakapozipata watoto wake kwa kuwa hiyo ilikuwa kama hati ya urithi wao. Mwandishi anasema:

> Bwana Msa anasema, " kaa tayari kwa kufanya kazi...Ingia katika pango lile ukatoe mali ya marehemu Bwana Hakimu!"...Spekta Seif alikwenda mpaka kunako lile pango katika jabali akapekenyapekenya matawi na majani huku na mpaka akapata pengee la kupita kwenye upenyo wa lile pamgo, akapita ndani. Alikaa kiasi cha dakika mbili kule ndani kimya; halafu-"- Bwana Msa, nipokee," ilitoka sauti yake kunako, domo la pango na Bwana Msa akasogea kumpokea... (kur. 65-66).

Dondoo hili linaonesha namna jamii za Kiafrika zinavyothamini pango kama sehemu ya maficho kwao. Kuoneshwa kwa Bwana Hakimu kuficha mali katika pango kunadhihirisha nguvu iliyopo katika ardhi ambayo kwa fikra za kiontolojia, watu huamini kuwa mapango yana uwezo wa kuhifadhi na kulinda mambo ya jamii husika.

Pia, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, MSA anaonesha wahalifu wakijificha kwenye pango la Giningi baada ya kumuua Mwanaginingi. Pango hilo linasadikiwa kuwa ni Mangapwani ambalo watu huenda kutoa kafara mbalimbali ili wafanikiwe mambo yao (Khamis, 2022). Mwandishi kuonesha Mwanaginingi kuuawa katika pango na wahalifu kujificha, hapo ina maana kiontolojia. Hii inamaanisha kuwa damu iliyomwagika ni ishara ya kafara zinazotolewa katika maeneo hayo. Hapa ni kuukilia kuwa mapangoni humo kuna nguvu inayoweza kuondoa uhai wa mtu au kuhifadhi jambo kwa kutegemeana na manuizo ya kafara zinazotolewa na wanajamii. Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inasisitiza uzingativu wa kani inayohusishwa na Mungu Mkuu, ndio maana nguvu ya pango katika jamii za Kiafrika huweza kuwapambanua wao na wanajamii wengine katika jamii pana waishio.

Halikadhalika, imebainika kuwa, sehemu hizi zenye miti, mito na mapango zinazotumiwa kwa ajili ya ibada, huitwa panga. BAKIZA (2010) wanasema kuwa, panga ni pahali kama chini ya mti au pangoni ambapo watu huenda kutambika. Akifafanua kuhusu mizimu, Makame (2016) anataja mapango kuwa ni sehemu zinazotumiwa kama panga. Naye, Hassan (2018) anafafanua sehemu nyingine zinazotumika kama panga kuwa ni pamoja na: miti mikubwa, mikusanyiko ya maji mengi, vichaka, milima na makaburi. Khamis (2022) anafafanua kuhusu panga kuwa, kupitia maeneo hayo watu wanaweza kutatuliwa matatizo yao. Inaaminika kuwa ndani ya panga kuna mashetani na majini ambao ni viumbe vilivyoumbwa na *Allah*. Majini ni kama vile Subiani, Ruhani, na hata vibwengo; na mashetani watu ni wale wanaotumia hayo mashetani na majini (Sengo, 1995).

Panga kwa jamii ya Wazanzibari, ni muhimu kwa sababu huwasaidia watu kuchagawa na kuweza kuagua mambo mbalimbali yanayowasibu. Wakati mwingine hupata hata mapendekezo ya dawa za kutibu matatizo hayo. Kwa

kuthibitisha hili, katika riwaya ya *Kisima cha Giningi*, mwandishi ameonesha jinsi watu walivyokuwa wanakwenda kuomba katika panga ya mzimu Habusa wakiamini kuwa shida zao zinatatuliwa kupitia yeye. Haya yanabainika pale MSA anaposema, "Watu wengi huja kuweka nadhiri, wakaomba maombi yao wayatakayo kwa jina la Habusa, na inasemekana kuwa kila liombwalo kwa jina lake hupatikana" (uk. 68). Dondoo hili linadhihirisha nguvu ya panga ambazo hutumiwa katika jamii za Kiafrika. Hii ni kutokana na ukweli kwamba, kiontolojia maeneo hayo huwa na nguvu inayosababisha uwezo wa kuwasaidia watu kufanikiwa katika shughuli zao za kila siku.

Dondoo hili linadhihirisha kani ardhi kupitia mapambo yake ambayo kwayo hutengeneza panga. Inasadikika kuwa panga zina nguvu zinazotokana na mizimu inayoaminiwa kuwa ndiyo inayoweza kutatua matatizo yao. Wanajamii wanapokwenda kuomba katika mizimu hiyo, nguvu iliyopo kwayo huwezesha kutatua matatizo hayo (Madumulla, 1995). Hivyo, kuamini kwao kunatokana na kutekelezwa au kutatuliwa kwa matatizo yanayowakabili. Uwapo wa mapambo haya na matukio yanayotendeka ndani yake kunadhihirisha nguvu ya ardhi inayotawala uhai wa maisha watu.

Pambo jingine linalodhihirisha kani ya ardhi kiontolojia kwa jamii ya Wazanzibari ni bahari. Eneo la bahari katika Zanzibar ni mojawapo ya maeneo ya bahari ya Hindi. Bahari hiyo imepambwa na fukwe nzuri na mafungu ambayo huchomoza maji yanapokupwa (yanapotoweka). Pia, bahari hiyo ina miamba, majabali na mikoko ambayo inavutia kila jicho la mtazamaji (Mahmoud, 2020). Imebainika kuwa, bahari ni pambo mojawapo la ardhi lenye kudhihirisha kani ya kiontolojia kwa jamii ya Wazanzibari ambao huitumia kani ya bahari katika masuala ya kilimo na uvuvi kwa lengo la kujikimu katika maisha yao (Khamis, 2008). Katika kilimo, Wazanzibari hupanda mwani na kufuga samaki na pweza. Kwa upande wa uvuvi, watu huitumia bahari kama sehemu yao ya kupata kipato. Uvuvi hufanywa kwa kutumia mashua, boti, ngalawa na vidau. Wavuvi huvua kwa kutumia nyavu, madema na zana za moto (Khamis, 2022).

Inaaminika kuwa, kani ya uhai iliyopo baharini ni nzuri kwa sababu watu hujipatia kipato na chakula; kwa upande mwingine, ni mbaya kwa sababu inakula watu. Khamis (2022) anasema, "Kwa kweli, bahari tunaipenda, lakini inakula watu kila uchao. Sijui kuna siri gani ndani yake?" Imani ya Wazanzibari kuhusu ubaya wa bahari imetokana na kuamini kisa juu ya Mtume Nuhu. Kipindi hicho cha Nuhu, kinaelezwa kuwa kulitokea gharika katika bahari na watu wengi wakamezwa ndani yake. Vilevile, wanaamini juu ya kisa cha Mtume Yunus ambaye inasimuliwa kuwa alimezwa na samaki (aina ya chewa) baada ya kutumbukia baharini (Mkelle, 1972). Hili linasadifu mawazo ya Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika juu ya kuwapo kwa kani ya uhai inayotokana na Mungu Mkuu, miungu na mizimu. Hili linadhihirisha ukweli wa kuwapo kwa kani uhai katika bahari

inayotumiwa na jamii ya Wazanzibari. Imani yao kuhusu ubaya wa bahari, imetokana na yale yaliyoaminiwa tangu enzi za Mitume na kwamba hali bado ndivyo ilivyo kuhusu bahari. Masuala haya ya hatari ya bahari yamezungumziwa na mwandishi katika riwaya yake ya *Kisima cha Giningi* kwa kusema:

> "Leo kijana mmoja aitwaye Mshenga Hamadi wa Kidoti", alisema mtangazaji, "mmoja katika wale watu wawili tuliotangaza wiki iliyopita kuwa wamepotea baharini walipokwenda uvuvi, amerejea kwao mzima. Anasema siku kumi zilizopita waliingia katika ngalawa yao yeye na bwana mmoja aitwaye Ali Makame, maarufu hapo Giningi, kwa dhamiri ya kwenda kuvua. Baada ya wakati, ilitokea dhoruba kubwa na wakafanya shauri ya kutia nanga baharini, na wao waogelee… Jana katika wakati wa saa kumi alasiri, kwenye pwani ya Giningi, aliokotwa maiti ya mtu hapo ufukweni. Watu wanayemjua waliweza kusema maiti huyo alikuwa ni yule bwana Ali Makame wa Giningi aliyekuwa na Mshenga Hamadi wa Kidoti aliyerudi kwao leo. Maiti huyo alikuwa amekwisha chokolewa macho yote mawili na samaki na vilevile nyama ya mwili wake ilikuwa haijishiki… (kur. 89-90).

Dondoo hili linadhihirisha kuwapo kwa kani katika bahari, ambapo pamoja na kutumiwa katika shughuli za uvuvi, bado kuna baadhi ya hatari zinazoweza kutokea. Miongoni mwa hatari hizo ni kuzama, kupotea, kuliwa na samaki na hata kupoteza maisha. Nadharia ya Ontolojia ya Kiafrika inadadavua vyema masuala haya kuwa yanatokana na kuwapo kwa nguvu ya uhai inayotokana na Mungu Mkuu, miungu na mizimu. Nguvu hii kwa misingi ya imani ya jamii ya Wazanzibari inapatikana kupitia bahari yao inayowazunguka. Hili linaukilia kuwa, MSA hajayatoa katika ombwe mambo aliyoyaeleza katika riwaya zake, bali amedhihirisha kani ya ardhi ya Wazanzibari kiontolojia. Kwa msingi huo, mbali na kuwapo kwa mapambo yanayodhihirisha kani ya ardhi katika jamii ya Wazanzibari kiontolojia, kuna matumizi ya ardhi hiyo yanayodhihirisha zaidi kani hiyo.

### 5.3 Matumizi ya Ardhi Kiontolojia

Ardhi ni miongoni mwa vipengele vya msingi katika maendeleo ya maisha ya watu. Watu huitumia ardhi katika kuendesha maisha yao ya kila siku. Fikra za Wazanzibari kuhusu ardhi ni kwamba wanaichukulia kama uhai wao. Pia, inawaongoza katika ibada zao na kuwawezesha kujikimu katika mazingira yanayowazunguka. Hapa ina maana kwamba, ardhi ina kani uhai inayowasaidia katika kuishi na uwapo wao (Khamis, 2022). Imebainika kuwa ardhi ya Wazanzibari inatumiwa katika masuala ya kilimo na shughuli nyingine. Wazanzibari wanaamini kuwa kilimo ndio msingi wa maisha. Idadi kubwa ya jamii yao inaishi kwa kutegemea shughuli za kilimo hasa katika maeneo ya shamba. Kilimo chao kimegawanyika katika mazao ya biashara na mazao ya

chakula. Miongoni mwa mazao ya biashara ni mikarafuu hasa huko Pemba, na minazi huko Unguja. Mazao ya chakula ni pamoja na mpunga, mihogo, migomba, magimbi, viazi vikuu na viazi vitamu. Mazao yote hayo hulimwa bila ya kutumia mbolea ya viwandani, na badala yake hutumia mbolea ya wanyama wafugwao majumbani kama vile kuku, mbuzi, kondoo au ng'ombe. Kwa mbogamboga, Wazanzibari wanajihusisha na kilimo cha tungule, biringani, bamia, mchicha, vitunguu na mtoriro. Wanazithamini mbogamboga kwa kuwa wanaamini kuwa ndizo zinazoongeza nguvu katika miili yao (Khamis, 2022).

Maelezo hayo yanashabihiana na ya Ameir (2011:11-14) anayesema: "MSA alikuwa mchumi kwa sababu ameweza kuyasawiri mazao ya biashara na yale ya chakula katika riwaya zake". Nukuu hii inaonesha kuwa pamoja na kuwa mchumi, pia aliijua vyema kani ya ardhi yake na vyakula vinavyopatikana katika jamii yake. Ameyasawiri haya kupitia riwaya yake ya *Kisima cha Giningi*. Kwa mfano, anataja baadhi ya mbogamboga na mazao ya biashara kwa kusema kuwa:

> Bustani yake Spekta Seif ilikuwa nzuri ingawa ndogo; kwani, kwa kiasi chake yeye mwenyewe tu, ilikuwa inamtosha; hahangaiki kutafuta mboga. Nyanya, tungule, biringani, bamia, kitunguu maji na thaumu – mimea yote hiyo ilikuwa imestawi… (uk. 12).

> Lakini kwa kutaka kuondosha huo mzozo – ikiwa itasaidia – nimemkatia katika shamba hili mikarafuu mia na minazi mia, na nimemwandikia waraka rasmi (uk. 22).

Madondoo haya yanaonesha mazao yanayolimwa katika jamii ya Wazanzibari kuwa ni pamoja na minazi na mikarafuu ambayo ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa Wazanzibari. Kuelezwa kwa mazao haya, mwandishi ameidhihirisha kani ya uhai iliyopo katika jamii yake kiontolojia. Masuala ya kiuchumi ya jamii husika hudhihirisha uhai wa jamii hiyo. Haya ni miongoni mwa masuala muhimu ya jamii ambayo ameweza kuyadhihirisha kwa lengo la kuitambulisha jamii yake kwa jamii nyingine za Kiafrika na nje ya Afrika. Kwa kufanya hivyo, riwaya zake zimekuwa miongoni mwa riwaya zinazoweza kuibua kani uhai ya matumizi ya ardhi ambayo ndiyo ya msingi katika kudhihirisha kuwapo kwa fikra za jamii yake kiontolojia.

Pamoja na hayo, matumizi ya ardhi yana kani katika kuendeleza uhai wa mtu baada ya kufa. Kiontolojia, kwa jamii ya Wazanzibari, mtu akifa mwili wake huwa hauna thamani tena ya kuishi ulimwenguni. Hivyo, ni lazima azikwe ili aende kuanza maisha mengine. Mussa (2020) anasema kuwa:

> Watu wanaokufa tunawazika kwa sababu ya utukufu walio nao. Hii inamaanisha [kuwa] mwanadamu si sawa na mnyama kwamba atupwe, la hasha! Akifa, anazikwa katika kaburi ambalo lina urefu wa kutosha ili kuzuia wanyama wasije wakamfukua. Shimo la kaburi huwa pima

> ya mkono kwenda chini na lina mwanandani. Hapo kwenye mwanandani ndipo maiti huwekwa kisha hufunikwa kwa ubao mpana unaolingana na sehemu husika. Kabla ya hayo yote, huwa tayari kashaoshwa na kuvishwa sanda.

Maelezo haya yanaonesha jinsi matumizi ya ardhi yanavyodhihirisha kani ya uhai kwa mwanadamu aliyekufa. Kiontolojia, kwa jamii ya Wazanzibari mtu akishakufa, kuzikwa ni lazima. Kwa desturi mtu akishakufa huwa hana tena umuhimu wa kuishi katika ulimwengu wa walio hai (Sengo, 2008). Hata hivyo, huwa na utukufu unaosababisha azikwe kwa utaratibu maalumu. Utaratibu huo husaidia kumsitiri kwa kuogopa kuliwa na wadudu na wanyama wa porini. Aidha, kupitia nguvu ya uhai iliyopo katika ardhi, Wazanzibari wanaamini kuwa mtu aliyekufa anaweza kuwa katika sehemu salama ilimradi aliishi kwa wema na/au vinginevyo kama aliishi kwa ubaya. Makala haya yanaona kuwa, kuwapo kwa fikra za kuendelea kuishi kwa mtu aliyezikwa katika ardhi, kunadhihirisha kuwapo kwa kani ya ardhi ambayo inahusishwa na kuwapo kwa kani ya uhai inayotokana na Mungu Mkuu, miungu na mizimu.

## 6.0 Hitimisho

Kwa jumla, tunaweza kusema kuwa, wanadamu na mazingira yanayowazunguka ni vipengele vya ontolojia vinavyodhihirisha kuwapo kusiko kwa lazima. Hapa ni kusema kuwa, kuwapo kwa wanadamu na mazingira yao ni jaala ya kuwako kwa lazima, ambayo ni Mwenyezi Mungu. Kiontolojia, kwa Waafrika, suala hili linatiliwa nguvu na kuwapo kwa msingi unaosisitiza kuwa, kuna kani ya uhai inayohusishwa na Mungu Mkuu. Hivyo, kipengele cha ardhi kinakamilishwa na mapambo kama vile panga na bahari na matumizi kama vile kilimo na kuzikana. Vipengele hivyo vinadhihirisha kani uhai iliyopo katika ardhi husika. Kwa muktadha huo, riwaya za MSA zimedhihirisha kani ya ardhi kiontolojia katika jamii ya Wazanzibari, kwa kuwa zimebainisha na kufafanua ukweli juu ya fikra za Wazanzibari kuhusu kuwapo kwao na mazingira yanayowazunguka. Kwa jumla, kila jamii ina mambo yake ambayo ndiyo hudhihirisha ontolojia yao. Jamii ya Wazanzibari, fikra za kuwapo kwao zinadhihirishwa na kani ya kipengele cha ardhi yao kupitia mapambo na matumizi yake.

## Marejeleo

Abdulla, M. (1973) *Duniani Kuna Watu*. Nairobi: East African Publishing House.

Abdulla, M. (1984) *Kosa la Bwana Msa*. Zanzibar: Masomo Bookshop.

Abdulla, M. (1958) *Kisima cha Giningi*. Nairobi: Evans.

BAKIZA (2010) *Kamusi la Kiswahili Fasaha*. Nairobi: Oxford University Press.

Carazzon, R. (2010) "Birth of New Science: The History of Ontology from Suarez to Kant". *History*. Inapatikana katika www.ontology.co. Iliyosomwa tarehe 12 Desemba 2018.

Chuachua, R. (2016) *Falsafa ya Riwaya za Shaaban Robert na Euphrase Kezilahabi Katika Muktadha wa Epistemolojia ya Kibantu*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Cohen, L., Manion, L. na Morrison, K. (2007) *Research Methods in Education* (6thed). London: Routledge.

Cresswell, J. (2002) *Educational Research: Planning, Conducting and Evaluating Quantitative and Qualitative Research*. New Jersey: Merrill Prentice-Hall.

Hassan, H. R. (2018) *Ujaala katika Ushairi wa Kiswahili: Mifano kutoka Tungizi za Mnyagatwa na Diwani ya Midulu*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Kagame, A. (1956) *The Rwandeese Bantu Philosophy of Being*. Brussels: Johnson Reprint Corparation.

Kajosi, S. (2013) *Suala la Uzazi katika Ontolojia ya Kibatu na Jinsi Lilivyojitokeza katika Riwaya za Kiswahili*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Kaponda, G. (2018) *Ontolojia ya Kiafrika katika Mbolezi za Wanyasa*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Khamis, A.A. (2008) *Jadi na Utamaduni wa Mswahili wa Zanzibar*: *Utamaduni wa Mzanzibari*. Zanzibar: BAKIZA.

Khamis, T.Y. (2021) "Mdhihiriko wa Mwanadamu kama Kipengele cha Ontolojia ya Kiafrika katika Riwaya Teule za Kiswahili". *RUJASS,* Juz. 7: 230-244.

Khamis, T.Y. (2022) *Mdhihiriko wa Ontolojia ya Wazanzibari katika Riwaya ya Kiswahili: Mifano kutoka Riwaya Teule za Muhammed Said Abdulla*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamivu (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Makame, S. (2016) Matumizi *ya Falsafa ya Usihiri katika Riwaya Teule za Euphrase Kezilahabi*. Tasinifu ya Shahada ya Uzamili katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Makumba, M. (2005) *Introduction to Philosophy*. Nairobi: Paulines Publication.

Masolo, D. (2011) *African Philosophy in Search of Identinty*. Bloomington: Indiana University Press.

Mbiti, J. (1969) *African Religion and Philosophy*. London: Heineman.

Mbiti, J. (2015) *Introduction African Religion*. Heineman: University of Michighan.

Merriam, S. (1998) *Qualitative Research and Case Study Applications in Education*. San Fransisco: Jossey-Bass Publishers.

Mihanjo, A. (1997) *Falsafa na Ufunuo wa Maarifa: Toka Uyunani hadi Afrika*. Morogoro: Salvatorianum.

Mihanjo, A. (2004) *Falsafa na Usanifu wa Hoja- kutoka Wayunani hadi Watanzania* (*Waafrika*). Morogoro: Salvatorianum.

Mjawiri, M. (2011) "Muhammed Said Abdulla, Jamii, Maisha yake na Utajiri wa Kazi zake". *Makala za Semina ya Kumuenzi Muandishi Muhammed Said Abdulla*. *Jahazi,* Juz.1 (1): 109-115.

Mkelle, B.M. (1972) *Utenzi wa Nabii Yunus: Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mor, C. (2001) *A Matter of Fate*: *The Concept of Fate in Arabs World as Reflected in Modern Arabic Literature*. Oxford: Oxford University Press.

Mpalanzi, L. (2019) *Ujitokezaji wa Falsafa ya Kifrika katika Riwaya za Kiethinografia. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili* (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dar es Salaam.

Mulokozi, M. (2017) *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili: Kozi za Fasihi Vyuoni na Vyuo Vikuu.* Dar es Salaam: KAUTTU.

Ngangah, I. G. (2019) "Vital Force, Personhood, and Community in African Philosophy". *An Ontological Study*. Inapatikana katika https://Dol:10'24940/theijhss/2019/v7/i10/HS/HS1910-023. Ilisomwa tarehe 20/5/2025.

Sengo, T.S.Y. (1995) *Itikadi katika Jamii za Kiswahili*: *Lugha*, *Utamaduni na Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Sengo, T.S.Y. (2008) *Tafakuri ya Utu na Uhai*. Dar es Salaam: Huda Publishers.

Temples, P. (1959) *Bantu Philosopy*. Paris: Presence Africaine.

Toufik, M. (2019*) Ukwepi na Uhalisi wa Riwaya za Muhammed Said Abdulla katika Muktadha wa Maisha ya Karne ya 21*. Tasinifu ya Shahada ya Umahiri katika Fasihi ya Kiswahili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, Zanzibar.